# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KILIMANJARO
Anwani ya Simu:'REGCOM'KILIMANJARO
Simu Na. Moshi 027-2754236/7, 027-2752184
Barua Pepe: ras@kilimanjaro.go.tz
: ras.kilimanjaro@tamisemi.go.tz
Nukushi Na. 027-2753248
Unapojibu tafadhali taja:

OFISI YA MKUU WA MKOA,
17 BARABARA YA FLORIDA,
S.L.P. 3070,
**25107 MOSHI.**

***Kumb. Na***.BD.54/247/AD/04/02

17 Aprili, 2023

Meneja Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC)
Kanda ya Kaskazini,
S.L.P 3070
**MOSHI.**

**YAH: UWEKEZAJI WA KAMPUNI YA MACJARO KWENYE MASHAMBA YANAYOMILIKIWA NA VYAMA VYA USHIRIKA MKOANI KILIMANJARO.**

Somo tajwa hapo juu la husika.

2. Rejea barua yako iliyokuwa na Kumb. Na.DA.201/234/01/20 ya tarehe 20/02/2023 kuhusu uwekezaji wa Kampuni ya MACJARO Ltd kwenye Mashamba yanayomilikiwa na Vyama vya Ushirika vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya Siha (Koboko AMCOS) na Halmashauri ya Wilaya ya Hai (Mradi wa Pamoja Lemmkinna Joint Enterprises Ltd na Machame Mkuu AMCOS). Ufuatiliaji umefanyika na majibu yamepatikana kutoka kwenye vyama husika na majibu yameambatishwa na barua hii.

3. Ukiri huo umeambatishwa pamoja na barua hii. Ni muhimu ukiri usomwe kwani LEMMKINA ENTREPRISES JOINT LTD kuna kiashiria cha mgororo.

4. Nashukuru kwa ushirikiano,

Dkt. Vedast M. Makota
**K.n.y. KATIBU TAWALA WA MKOA**

LEMMKINA JOINT ENTERPRISES LTD,

S. L. P 159,

**HAI.**

30/03/2023

KATIBU TAWALA,

OFISI YA MKUU WA MKOA,

S. L. P 3070,

**MOSHI.**

K.K AFISA USHIRIKA,

WILAYA YA HAI,

S. L. P 27,

**HAI.**

Inapitishwa wasaidiwe

DISTRICT CO-OPERATIVE OFICER
P. O. Box 27 - HAI
DATE: 04/04/2023
SIGN:

**YAH:- MIKATABA YA UPANGISHAJI WA MASHAMBA KATI YA KAMPUNI YA MACJARO LIMITED NA CHAMA CHA USHIRIKA CHA LEMMKINNA JOINT ENTERPRISES LIMITED.**

Somo tajwa hapo juu lahusika. Pamoja na barua yako ya tarehe 07/03/2023 kutaka vyama vyenye mikataba na kampuni ya Macjaro Limited kuthibitisha endapo kama kuna mgogoro wowote kati ya kampuni na chama.

Bodi ya LEMMKINNA inathibitisha kuwa kwa sasa hakuna mgogoro wowote ila kuna kiashiria cha mgogoro kwani hadi tarehe ya kuandikwa kwa barua hii kampuni ya Macjaro Limited imekiuka mkataba kuhusu taratibu za kulipa kodi ya pango ambayo kimkataba inatakiwa kulipwa Januari ya kila mwaka. Hakuna utaratibu wa kulipa nusu. Hadi tarehe ya barua hii amelipa nusu ya kodi ya pango.

..............................

**TEREWANDUMI PH. SWAI**

**MWENYEKITI WA BODI**

LEMMKINNA CO-OPERATIVE JOINT ENTERPRISES LTD.
P.O. Box 1484 MOSHI

**Nakala:-** Mkurugenzi Kampuni ya Macjaro - Kwa taarifa.

b) Uthibitisho kutoka chama cha Ushirika LEMMKINA Joint Enterprises wamethibitisha kwamba kwa sasa hawana mgogoro ila wameona kuna kiashiria cha mgogoro kwani hadi tarehe 30/03/2023 mwekezaji wao MACJARO Limited amekiuka Mkataba kuhusu taratibu za kulipa kodi ya pango ambayo kimkataba inatakiwa kulipwa yote Mwezi Januari kwa kila mwaka bali yeye amelipa nusu ya kodi ya pango na nakala ya uthibitisho huo imeambatanishwa katika barua hii.

Kwa barua hii ninakuomba uwapatie msaada wowote wanaohitaji wadau wetu wa Ushirika kutoka Wilaya yetu ya Hai Mkoani Kilimanjaro.

Nakutakia Utekelezaji mwema.

"Ushirika hujenga Ulimwengu ulio Bora"

DISTRICT CO-OPERATIVE OFICER
P. O. Box 27 HAI
DATE 04/04/2023
SIGN

.................................

**SWAI O. ERASTO**

**AFISA USHIRIKA (W) HAI**

NAKALA KWA:

1. MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI (W) HAI (AIONE KWENYE FAILI).

MACHAME NKUU AMCOS

S.L.P 659-MOSHI.

27/03/2023

KATIBU TAWALA

MKOA WA KILIMANJARO

S.L.P 3070-MOSHI

K.K

AFISA USHIRIKA

WILAYA YA HAI

S.L.P 27

DISTRICT CO-OPERATIVE OFICER
P. O. Box 27 - HAI
DATE: 27/03/2023
SIGN:

YAH: UTHIBITISHO WA KUTOKUWA NA MGOGORO NA MWEKEZAJI MACJARO LTD

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

Chama cha Machame Nkuu AMCOS ambacho kinamiliki shamba la Mkufi Estate kinakiri kutokuwa na mgogoro na mwekezaji wake MACJARO LIMITED ambae amewekeza katika shamba la Mkufi Estate kuanzia mwaka 2021.

Nakutakia utekelezaji mwema.

Pamoja Tujenge Uchumi.

CHRISTOPHER LEMA

MWENYEKITI MACHAME NKUU AMCOS

MACHAME NKUU AGRICULTURAL MARKETING CO-OP. SOCIETY LTD
REG NO. ...
P. O. Box 659 ... HAI

KOBOKO AMCOS LTD,
S.L.P 110,
SANYA JUU.
SIHA.

3)

14/03/2023

OFISI YA MKUU WA MKOA,
17 BARABARA YA FLORIDA,
S.L.P 3070,
25107 MOSHI
K.K
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

YAH: **MKATABA WA UPANGISHAJI WA SHAMBA KATI YA KOBOKO AMCOS NA KAMPUNI YA MACJARO LTD.**

Rejea barua yako yenye Kumb. Na BD.54/247/04/94 ya tarehe 07/03/2023.

Kwa barua hii tunapenda kukufahamisha kwamba chama cha Ushirika cha msingi Koboko (AMCOS) ndiyo wamiliki halali wa Pyrita lenye ukubwa wa Ekari 200, lenye TITLE NO.11331 FARM NO. 316/4 lililoko katika Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro.

Mnamo mwaka 2021 Wanachama wa chama hiki kupitia Mkutano wao Mkuu walipiga kura kwa kauli moja na kukubaliana kuwa Bodi ya Chama cha Msingi Koboko Amcos iingie Mkataba na Kampuni ya Macjaro Ltd ambao ulisainiwa tarehe 01/10/2021.

Muda wote huo Kampuni ya Macjaro Ltd imekuwa ikifwata sheria na taratibu zote zilizopo kwenye Mkataba wa Makodisho ya Shamba kwa kulipa Kodi kwa wakati na kufuata mpango wa maendeleo kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba.

Kupitia barua hii tunapenda kufahamisha kuwa hatuna mgogoro wowote kati ya Koboko Amcos na Macjaro Ltd

**"PAMOJA TUJENGE UCHUMI WENYE NGUVU NA ENDELEVU"**

| | | |
|---|---|---|
| SAMSON A. MASERI | KOBOKO RCS. LTD<br>KLR/222<br>BOX 110 SANYA JUU<br>SIHA | JOHN I. MMARI |
| MWENYEKITI | | KATIBU |